**MTIHANI WA KUFUNGUA MUHULA WA 2 - 2024**
**KISWAHILI**
**KIDATO CHA NNE**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**SEHEMU YA A. UFAHAMU (ALAMA 15)**

**Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali yanayofuata.**

Suala la mahusiano ya wanadamu katika jamii, uainishaji wake na udhihirikaji wake limewashughulisha wataalamu wa elimu jamii kwa dhari ya miaka. Suala huwatafakarisha wataalamu hao kutokana na umuhimu wake katika maisha ya binadamu. Msingi mkuu wa uainishaji wa mahusiano hayo ni kukichuza kipindi cha mahusiano yenyewe. Yapo mahusiano baina ya waja ambayo yanachukua muda mfupi, kwa mfano saa au dakika chache, na mengine ambayo huenda yakachukua miaka ayami.

Mahusiano ya muda mrefu kabisa ni yale yanayojulikana kama mahusiano ya kudumu. Inamkinika kudai kuwa miundo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi huweza kuyadhibiti mahusiano hayo kwa kiasi kikubwa. Watu wengi huitakidi kuwa uhusiano uliopo baina ya mtu na jamaa yake utachukua muda mrefu, na kwak hiyo ni uhusianok wa kudumu. Hali hii utokana na uhalisi kuwa tunahusiana na jamaa zetu kwa kipindi kirefu labda tangu ukembe hadi utu uzima wetu. Uhusiano huu hautarajiwi kuvunjwa na umbali wa masafa baina yetu; tunaendelea kuwasiliana kwa barua au katika enzi hii ya utandawazi, kwa kutumia nyenzo za teknohama kama mtandao na simu za mkononi, na kudumisha uhusiano wetu wa kijamaa. Hata hivyo, inawezekana baadhi ya mahusiano ya kijamaa yasiwe ya kudumu. Mathalan, uhusiano uliopo baina ya mke na mume, na ambao unatarajiwa kuwa wa kudumu au wa kipindi kirefu, unaweza kuvunjwa kwa kutokea kwa talaka. Talaka hiyo inavunja ule uwezekano wa uhusiano wa kudumu unaofumbatwa na sitiari ya pingu za maisha.

Katika ngazi ya pili, mahusiano ya kipindi cha wastani, kuna mahusiano yanayohusisha marafiki z etu maishani, shuleni au kwenye taasisi zote zile, majirani zetu, wenzetu katika mwahali mwa kazi, washiriki kwenye sehemu za ibada au za burudani na wenzetu kwenye vyama tofauti na makundi ya kujitolea. Inawezekana kudahili kuwa baadhi ya mahusiano haya, hususan baina ya marafikina majirani huweza kuwa yamiongo na daima. Hali hii huweza kutegemea muundo na mfumo wa jamii. Kwa mfano, kwa wanajamii wanaoishi kwenyejanibu fulani mahsusi, na kwa miaka tawili bila ya kuhajiri, uhusiano wao na majirani huwea kuwa wa kudumu. Hali hii inasigana na hali iliyoko kwenye maisha ya mijini. Maisha ya mijini yana sifa ya kubadilikabadilika. Isitoshe, kutokana na mfumu wa maisha ya kibepari yameghoshi ubinafsi mwingi. Mawimbi ya mabadiliko na ubinafsi huweza kumomonyoa ukuta wa uhusiano wa kudumu.

Mwelekeo wa maisha ya siku hizi ya uhamaji kutoka maeneo au viambo walikoishi watu unasababisha kupombojea kwa mahusiano ya kudumu baina yao na majirani zao. Uhusiano kati ya wenza katika mazingira ya kazi unahusiana kwa kiasi fulani na ule wa majirani. Vimbunga vya ufutwaji kazi, ubadilishaji wa kazi, hali zisizotegemewa na mifumo yua kimataifa pamoja na hata mifumo ya kisiasa huweza kuathiri mshikamano wa wanaohusika kazini. Kiwango cha mwisho cha mahusiano ni uhusiano wa mpito au wa muda mfupi. Mahusiano ya aina hii hujiri katika muktadha ambapo pana huduma fulani. Huduma

Mwelekeo wa maisha ya siku hizi ya uhamaji kutoka maeneo auviambo walikoishi watu unasababisha kupombojea kwa mahusiano ya kudumu baina yaona majirani zao. Uhusiano kati ya wenza katika mazingira ya kazi unahusiana kwa kiasi fulani na ule wa majirani. Vimbunga vya ufutwaji kazi, ubadilishaji wa kazi, hali zisizotegemewa na mifumo yua kimataifa pamoja na hata mifumo ya kisiasa huweza kuathiri mshikamano wa wanaohusika kazini. Kiwango cha mwisho cha mahusiano ni uhusiano wa mpito au wa muda mfupi. Mahusiano ya aina hii hujiri katika muktadha ambapo pana huduma fulani. Huduma hizi zinaweza kuwa za kukani, kwenye sehemu za ibada, kwenye kituo cha mafuta, kwa kinyozi, kwa msusi na kadhalika. Kuna sababu kadha zinazotufanya kuyazungumzia mahusiano ya aina hii kama ya mpito.

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Kwanza, uwezekano wa mabadiliko ya anayeitoa huduma hiyo ni mkubwa. Si ajabu kuwa unaporudi kwa kinyozi au msusi unatambua aliyekushughulikia hayupo. Hata hivyo, kuna vighairi hus就san pale ambapo mtoa huduma ayanayehusika ni Yule Yule mmoja.

Mahusiano ya mpito yanatawaliwa na 'uhusiano wa chembe chembe'. Uhusiano wa chembe chembe, bidhaa ya mfumo wa kibepari, unamaanisha kuwa kinachomshughulisha mtu ni chembe ndogo tuya mwenzake. Chembe hiyo inaweza kuwa huduma, kwa mfano, gazeti analokuuzxia mtu, viatu anavyokushonea, nguo anazokufulia, ususi anaokufanyia n.k. Mahusiano ya aina hii yametovukwa na hisia za utu nan i zao la mirumo ya kisasa ya kiuchumi na kijamii. Mtuanayehusiana na mwenzake kwa misingi ya chembe ndogo tu, huenda asijali kama mwenzake amekosa chakule, amefutwa kazi, amefiliwa, ameibiwa na kadhalika.
Suala kuu tunalopaswa kujiuliza ni: Je, tunahusiana vipi na jamaa zetutaasisi zetumarafiki zetu na majirani zetu? Je, uhusiano wetuna riaia wenzetu ni wa aina gani? Je, uhusiano wetu nan chi yetu ni wa mpito auni wa kudumu?

**MASWALI:**

(a) Taja kigezo muhimu cha kuzungumzia mahusiano. (alama 1)
- **Kukichuza kipindi cha mahusiano yenyewe.**

(b) Eleza imani ya watu kuhusu uhusiano baina ya jamaa. (alama 1)

- **Uhusiano baina ya jamaa ni wa kudumu. Haijalishi umbali wa masafa wanamoishi.**

(c) Fafanua athari ya teknolojia kwenye mahusiano ya watu. (alama 2)

- **Athari za teknolojia imeharibu baadhi ya mahusiano ya watu kama mke na mume.**

(d) Taja sifa kuu yamahusiano yamuda mfupi. (alama 2)
- **Mahusiano mafupi ni yale ya kudumu muda mfupikwa miktadha fulani kama ya kinyozi, ususi, ibada n.k.**

(e) Eleza sababu nne kuu za kuharibika kwa mhusiano katika maisha ya leo. (alama 4)
- **Mifumo ya kipepari mijini ya ubinafsi**
- **Mifumo ya kisiasa huathiri mshikamano wa uhusiano.**
- **Uhusiano wa kijamaa kati ya mke na mume huenda yasidumu.**
- **Kukaa mahali kwa muda mfupi hasa kwa chembe ndogo tu.**

(f) Je, kifungu, hikikin aujumbe gani mkuu? (alama 2)
- **Kifungu hiki ni kuhimiza watu kuwa na uhusiano mwema.**

(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika kifungu. (alama 3)

**(i) Inasigana – Inakuwa tofauti**

**(ii) Yameghoshi – Yamechakuwa/jaa**

**(iii) Vighairi – Vitu vya kubadilisha**

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

**SEHEMU YA B: UFUPISHO: (ALAMA 15)**

Soma makala haya kisha ujibu maswali yanayofuatia.

Mwelekeo wa utoaji mafunzo kwa mwaloimu wa shule za sekondari nchini unazua mjadala. Hatua katika Nyanja hizi zinaonekana kuchukuliwa bila kutilia maanani utabili wa idadi katika siku za usoni.

Hapo miaka ya tisini, walimu wengiwaliohitimukatika shahada za diggrii na diploma hawakuegemea upande wa hisabati, sayansi na lugha (Kiingereza na Kiswahili) Hivyo kukazuka kampeni za chini kwa chini katika vyuo vya nchi ambayo walimu – wanafunzi walihimizwa kusomea, Hesabati, Sayansi na lugha. Hili lilionekana kuwa suluhu kwa wakati ule kwani punde idadi ya marupurupu maalum maarufukwa jina "Special allowance" kwenye mishahara yao.

Idara za Dini, Historia na masomo mengine husika zilipuuzwa na idadi ya wanafunzi waliojisajili hapa kupunguka kabisa. Wnafunzi katika idara hizi walionekana kutokuwa na matumaini ya kuajiriwa kwani wenzao waliokwisha hitimu walikuwa wengi kupindukia.

Hali hii ilidumishwa na miaka ya karibuni imeshuhudia tatizo linguine tofauti; ubabe wa walimu wa Dini na Historia na ongezeko kubwa la walimu wa Hesabati, Sayansi na lugha. Dalili zake ni ukweli kwamba shule nyngi hazina walimu wa kutosha katika Dini na Historian a zinapotangaza nafasi hizi kuwa wazi hukuwa wanaoojitokeza kuzichukua. Miongoni mwa walimu waliohitimu na wanaosaka nafasi za kazi, asilimia kubwa zaidi ni wa Hesabati, Sayansi au lugha. Swali ni je, kwa nini mambo yabadilike haraka jinsi hii"?

Lawama zote zafaa kuandikiwa wizara ya Elimu hasa idara zinazohusika na tarakimu na utoaji wa mafunzo kwa elimu hasa idara zinazohusika na tarakimu na utoaji wa mafunzo kwa walimu. Kwa kufuata njia za kitaalamu, inawezekana kukadiria idadi ya walimu watakaohitajika katika masomo mbalimbali kwa kipindi cha miaka hamsini au hata zaidi. Maafisa katika idara hizi wafaa kuajibika na kutoa mwelekeo dhabiti ili kujepusha nchi matatizo kama hayo.

**MASWALI:**

(a) Fupisha aya ya kwanza na ya pili kwa maneno 50.

(alama 6, mtiririko 1)

**Nakala chafu**

- **Mwelekeo wa mafunzo ya walimu wa sekondari wazua mjadala.**
- **Mahitaji ya baadaye ya walimu hayatiliwi maanani**
- **Miaka ya tisini, waliohitimu hawakuegemea masomo ya Hesabati, Sayansi na lugha.**
- **Hivyo kampuni zikawa za kuhimiza walimu kusomea masomo**
- **Ilikuwa suluhu ya muda kwani walimu waliohitajika waliongezeka.**
- **Waalimu hawa walipewa nyongeza katika mishahara yao.**

(b) Ni hoja zipi muhimu zinazojitokeza katika aya ya tatu hadi ya mwisho? (alama 7, mtitiriko 1)

**Nakala chafu**

- **Idadi ya waliosomea masomo haya mengine ilipunguka**
- **Walonekana kutokuwa na matumaini ya kukajiriwa**
- **Hali hii iliendelea na tatizo lingine likachipuka**
- **Walimu wa Dini na Historia waliadimika**
- **Walimu wa Sayansi, Hisabati na lugha wakaongezeka na kukosa kazi**
- **Wizara ya elimu kulaumiwa kwa kutokadiria idadi ya walimu watakaohitajika.**
- **Maafisa wapaswa kutoa mwelekeo ili kuepuka matatizo haya.**

  - **(Hoja 7 x 1 = 7)**

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

**SEHEMU YA C: MATUMIZI YA LUGHA**

1. (a) Haya ni maneno gani?
   (i) Nazali ya ufizi, irabu ya chini kati, irabu ya chini kati, nazali ya midomo. (alama 1)
   **Naam**

   (ii) Mbele juu, mbele kati, nyuma juu na mbele kati. (alama 1)
   **Ieue**

   (b) Eleza sifa bainifu za sauti /h/ (alama 2)

   **Ni kikwamizo cha kooni**

   (c) Andika mifano ya sauti za mdomo-meno.

   **(i) /f/**

   **(ii) /v/**

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

2. Andika sentensi moja na "vile" kama kitenzi na kivumishi. (alama 2)
   **Vile** **Vile** **Vyakula**
   **T** **V**

3. Yakinisha sentensi hii: (alama 2)
   Jambazi baya halikuuawa kwa kupigwa risasi.

   **Jambazi baya liliuawa kwa kupigwa risasi**

4. Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo: (alama 2)
   **Ingawa shamba lake si kubwa, linatoa mazao tele.**

   **(i) Ingawa shambal lake si kumbwa – Kishazi tegemezi**

   **(ii) Linatoa mazao tele – Kishazi huru.**

5. Onyesha matumizi ya **PO** katika sentensi:
   (i) Alipoketi pana vumbi. - Mahali (alama 2)

   (ii) Aketipo watu humshangilia - Wakati wowote (alama 2)

6. Andika ukubwa wingi wa:
   Mbuzi alitoka katika shamba la mwanamke. (alama 3)

Mabuzi yalitoka katika majishamba ya majianajike.

7. Kanusha sentensi ifuatayo. (alama 2)
   Nyumba yake ina milango mikubwa na mapamba mengi.

   **Nyumba yake haina milango mikubwa na miembamba mingi.**

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

8. Eleza maana nne za sentensi ifuatayo. (alama 4)
Alinunuliwa ng'ombe na mtoto wake.

**(i) Mtoto alimpa baba ng'ombe.**

**(ii) Mtoto alimpa baba ng'ombe na ndama**

**(iii) Ng'ombe wake na mtoto wote walinunuliwa**

**(iv) Mtoto alinunua ng'ombe baba alitaka kuuza.**

9. Changanua sentensi kwa visanduku. (alama 4)
Wanafunzi wasiofanya mitihani watapata alama za kuudhi.

| S | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| KN | | KT | | | |
| N | S | T | N | H | V |
| Wanafunzi | Wasiofanya mtihani | Watapata | Alama | Za | kuudhi |

10. Iunde upya sentensi hii ukigeuza shamirisho kitondo kuwa kiima. (alama 2)
Tuna mwandalia mgeni chakula sasa hivi.

**Mgeni ataandaliwa chakula sasa hivi.**

11. Andika kwa udogo. (alama 2)
Tulipoyaona yalikuwa yakisoma majitabu.

**Tulipoviona vilikuwa vikisoma vijitabu.**

12. Neno "furaha" liko katika ngeli gani? (alama 2)

**Ngeli ya I - I**

13. Andika kinyume cha sentensi hii. (alama 2)
Watoto wanaombwa waanike nguo.

**Watoto wanalazimishwa kuanua nguo .**

14. Onyesha na uainishe mofimu katika neno: (alama 2)
Tulipowapitisha

**Tu – nafsi ya kwanza**
**li – wakati uliopita**
**wa – kirjeshi cha watendewa**
**pik – mzizi**

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

**ish – kauli yakutendesha**
**a - Kiishio**

**SEHEMU YA D: ISIMU JAMII**

(a) Eleza maana ya istilahi zifuatazo. (alama 2)

**(i) Sajili – Ni matumizi ya lugha katika muktadha fulani.**

**(ii) Lahaja – Ni vilugha vidogo vidogo vinavyopatikana katika lugha kuu kimaeneo.**

(b) Taja nadharia tatu za chimbuko la Kiswahili. (alama 3)

**(i) Kiswahili ni mojawapo wa lahaja ya Kiarabu. Haikupata mashiko nadhama hii**
**(ii) Kiswahili ni chimbuko la kizazi kati ya waarabu na waafrika pwani ya Afrika mashariki.**
**(iii) Kiswahili ni lugha kutoka kwa Wabantu wa Afrika mashariki.**

(c) (i) Eleza maana ya dhana usanifishaji. (alama 2)

- **Ni kuwa na Kiswahili aina moja kutokana na aina nyingi zilizokuwa zikiongewa pwani na sehemu za Afrika mashariki.**

(ii) Eleza dhima mbili za lugha rasmi. (alama 2)

- **Ni lugha ya Taifa ya Kenya na Tanzania**
- **Inatumika katika kueneza habari mikutanoni, redioni na magazetini.**
- **Inatumika mikutano mbalimbali ya kiserikali kueneza sera.**

(iii) Fafanua sababu mbili za usarufishaji wa Kiswahili. (alama 2)

- **Kuwa na lugha moja kuu iliyosafi.**
- **Kuandika vitabu watoto/wasomi**
- **Kuandika Biblia/Kurani watu wasome**
- **Kuhubiria neno la Mungu n.k.**

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes